

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

GOVERNMENT NOTICE No. 227

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO, 2014.

Jina na
mwanzo
wa
kutumi-
ka

Eneo la
matumi-
zi

Tafsiri

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za mwaka 2014, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.
3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwu vinginevyo; -
“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni mtumishi yeoyote wa Halmashauri ambaye atateuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
“Gulio” maana yake ni eneo au sehemu yoyote ya wazi au iliyojengwa, na imetengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao ya shamba na bidhaa zingine za viwanda kwa siku maalum;
“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo;
“Mazao” maana yake ni pamoja na mazao ya chakula, mazao ya biashara na mazao ya misitu na maliasili ambayo kwa kawaida huzalishwa au kupatikana katika eneo la Halmashauri;
“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeoyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;
“Mnunuizi” maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yoyote inayojishughulisha na ununuizi wa mazao katika eneo la Halmashauri kwa nia ya kufanya biashara;
“Muuzaji” maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yoyote inayojishughulisha na uuzaaji wa mazao katika eneo la Halmashauri.

Ushuru

- 4.-(1) Halmashauri inaanizisha na kutoza ushuru wa mazao kwa asilimia

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

GN. No.227 Contd.

tano ya bei ya mauzo ya soko kutoka kwa kila mnunuzi wa mazao kwenye eneo la Halmashauri.

(1) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi kabla ya kusafirisha mazao.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi aliyelipa ushuru kuhakikisha anapewa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika na atatakiwa kuionyesha kwa Afisa Muidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(3) Upimaji wa mazao utafanyika kwa mzani au kipimo chochote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri au mamlaka nyingine iliyowekwa kisheria.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi ye yeyote kupokea na au kusafirisha mazao ambayo hayajalipiwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi
wa
Wakala

5.-(1) Halmashauri inaweza kuteua Kampuni na Taasisi kuwa Wakala wa kukusanya kwa masharti yaliyoanishwa kwenye Sheria Ndogo hizi na Mkataba.

(2) Kila mnunuzi wa wakala atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu mazao aliyonunua.

(3) Kila Meneja , Mkurugenzi au mtu yeyote mwenye dhamana ya usimamizi wa kiwanda, shirika, chama cha ushirika anaweza kutangazwa kuwa wakala chini ya Sheria Ndogo hizi.

Usima-
mizi wa
masoko

6.-(1) Masoko yote ndani ya eneo la Halmashauri yatakuwa chini ya Afisa soko ambaye atasimamia uendeshaji wa masoko hayo.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi, muuzaji, au mtu yeyote kumzuia Afisa soko au Afisa Muidhiniwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Uanzish
aji wa
masoko
vijijini

7.-(1) Kila kijiji ndani ya Halmashauri kitatenga eneo maalumu na siku maalum kwa ajili ya kuuzia mazao ambapo wauzaji watauzia mazao yao katika eneo hilo.

(2) Wanunuzi wote wa Mazao watanunua mazao hayo katika eneo lilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa mazao.

(3) Wanunuzi wote wa mazao watasaini mikataba ya ununuzi na Halmashauri na kupewa kibali cha ununuzi.

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

GN. No.227 Contd.

(4) Mnunuzi au Kampuni ambayo haitasaini mkataba wa ununuzi wa mazao au kununua mazao bila kibali haitaruhusiwa kununua mazao katika eneo la Halmashauri.

Muda
wa
kusafiris
ha
bmazao
Makosa

8. Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi yejote kusafirisha mazao baada ya saa 1.00 jioni na kabla ya saa 12.00 asubuhi.

9. Mtu yejote atakuwa ametenda kosa iwapo:-

- (a) atasafirisha mazao bila kulipa ushuru;
- (b) kwa makusudi atamsaidia mnunuzi kukwepa kulipa ushuru;
- (c) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru
- (d) atasafirisha mazao nje ya muda ulioainishwa; na
- (e) atanunua mazao bila kuwa na leseni.

Adhabu

10. Mtu yejote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kwa kipindi cha miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI

<i>Na.</i>	<i>Aina ya Mazao</i>	<i>Kiasi cha Ushuru</i>
1.	Kahawa	5 asilimia ya bei ya mauzo
2.	Chai	5 asilimia ya bei ya mauzo
3.	Kakao	5 asilimia ya bei ya mauzo

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo
GN. No.227 Contd.

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo iliyogongwa katika Sheria Ndogo hizi kwa Azimio la Baraza la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo cha tarehe 5 Mwezi Septemba, 2013, na ilibandikwa mbele ya:-

IMELDA ISHUZA,
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

MECKSON MOSES MWAKIPUNGA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

NAKUBALI,

Dodoma
19 Mei, 2014

MIZENGO P. PINDA,
Waziri Mkuu